



KONGAMANO LA ISHIRINI NA SABA LA KISWAHILI

Bayreuth, tarehe 8 hadi tarehe 9 mwezi wa sita 2014

Tarehe 29, mwezi wa nne,
mwaka wa 2014

Wapendwa Waalikwa, Mabibi na Mabwana,

Leo tunawaletea barua ya pili ya mwaliko ikiambatanishwa na ratiba yetu ya **Kongamano la Kiswahili**. Mwaka huu, kongamano halitafanyika katika jengo la 'Iwalewa-House' kama kawaida lakini kwenye campus ya chuo kikuu (jengo la SWO; taz. ramani chini). Kongamano litaanza Ijumaa **tarehe 8** mwezi wa sita kuanzia saa mbili na nusu asubuhi. Kutakuwa na malipo ya usajili ya €15 kwa wasio wanafunzi na €10 kwa wanafunzi.

Kabla Kongamano la Kiswahili halijaanza, wageni na wenyeji wote wanaombwa wakutane pamoja siku ya Jumamosi, **tarehe 7** mwezi wa sita, saa moja jioni katika **mkahawa** unaoitwa 'Delphi' uliopo mjini katika Badstr. 14. Huko kutakuwa na chakula na vinywaji ambavyo watakaohudhuria watajinunulia wao wenyewe.

Siku ya Jumanne na siku ya Jumatano, **tarehe 10** na **tarehe 11**, warsha **Mienendo mipya ya Kiswahili** ('New Dynamics in Swahili Studies') inayoandaliwa pamoja na chuo kikuu cha Leipzig itafanyika. Ratiba ya warsha hiyo inaambatanishwa pia. Malipo ya usajili yatakuwa € 15 kwa wasio wanafunzi na € 10 kwa wanafunzi. Kwa wale ambao watakuwa wamelipa tayari kwa ajili ya Kongamano la Kiswahili, kuhudhuria kutakuwa ni bure.


Wakati wa warsha ya 'Mienendo Mipya', kongamano la watalamu wa masomo ya kiafrika ya lugha, fasihi na historia ('**21st Afrikanistentag**') litafanyika pia. Wageni wa Kongamano la Kiswahili na warsha ya 'Mienendo Mipya' wanakaribishwa pia kuhudhuria kwenye kongamano la 'Afrikanistentag' bila ya kulipa malipo ya ziada. Tutatuma ratiba yao muda si mrefu.

Kutakuwa na **hafla** za ziada: Kwa kwanza, siku ya Jumatatu, tarehe 9, filamu 'Creating Comoria' itaonyeshwa kwenye jengo la AI, ukumbi wa 33 (taz. ramani). Jumanne, tarehe 10, tunataka kukualikeni kwa viburudisho katika bustani ya chuo kikuu. Siku ya Jumatano, tarehe 11, kongamano la masomo ya Kiafrika Ujerumani ('VAD') litaanza na litaandaa 'Science Slam' itakayofanyika mjini (Forum Phoenix).

Mkitaka kuhudhuria kwenye **kongamano la VAD** siku ya Alhamisi tu, kwa sababu kutakuwa na mawasilisho mengi yanayohusu utalamu wa lugha na fasihi, hamuhitaji kulipa malipo yote ya usajili ya VAD. Muktaka kukunua 'Day-Ticket' ya € 30, tafadhali, mumwandikie doris.loehr@uni-bayreuth.de. Ratiba ya VAD inapatikana kwenye tovuti ifuatayo: <http://www.vad-ev.de/index.php?id=24&L=1>.

Maelezo machache ya ziada:

Makongamano yanafanyika **hapo:**



Njia ya kwenda university campus ni kama ufuatayo:

Kwa gari: tumia highway A9, uiache kwenye „Bayreuth Süd”, kuelekea „Universität“.

Anwani ya navigation system:

Universität Bayreuth, Universitätsstraße 30, 95440 Bayreuth

Kwa basi: Kutoka stesheni ya reli Bayreuth, panda basi inayoelekea ZOH (kituo kikuu cha mabasi). Basi lenye nambari 304 na basi lenye nambari 306 yanakwenda kwa chuo kikuu. Mushuke kwenye kituo “Universitätsverwaltung”; ambacho kiko mbele ya jengo la SWO.

Hakuna mikahawa ama hoteli karibu kwenye campus ya chuo kikuu. Lakini tutahakikisha kwamba tutakuwa na chai na kahawa ya kutosha. Halafu, mkahawa wa chuo kikuu („Mensa“) hautakuwa wazi siku ya Jumapili na Jumatatu kwa sababu tutakuwa na sikukuu. Kwa hivyo, **chakula** cha mchana kitaletwa siku ya Jumapili na siku ya Jumatatu. Siku ya Jumanne na Jumatano, „Mensa“ itakuwa ni wazi. Lunch cards ambazo ni lazima mkitaka kula lunch huko zitauzwa kwa €10 wakati wa kujiandikisha (€4 ni deposit; zitaregeshwa baadaye).

Kwa **malazi**, angalia orodha ya hoteli kwenye tovuti ifuatayo:

http://www.afrikanistik.uni-bayreuth.de/en/colloq/21_-Afrikanistentag-in-Bayreuth/Accommodation.pdf

Tutawaandikiwa wanafunzi walioomba wakaribishwe na wanafunzi wetu katika nyumba zao muda si mrefu.

Ikiwa una maswali ya ziada, musisite kuniandikia: swahili@uni-bayreuth.de

Karibuni sana!

Salamu nyingi,

Clarissa Vierke